

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baiskeli Dar es Salaam  
Tarehe 13 Octoba 2007**

**Waliohudhuria**

Ally Saidi Mohamedi  
Aseli Wilison  
Dominata Rwechungura  
Elaine Baker  
Filbert Mbecha  
Frank Peter Rioeyongeza  
Hamadi Hatibu Bwaja  
Juma Ali Salehe Jongo  
Jumanne Idd Selemani  
Kassim Bakari  
Musa Athumani Lahi  
Patrick Masinga  
Patrick Maziku  
Paulo Atibu Hatibu  
Sosthenes C Amlima  
Sudi Saidi Ramadhan  
Yusufu Juma

**Msafara wa Baiskeli**

Elaine alisema kwamba wiki hii ni Mejah alituatilia ufadhili wetu kutoka ubalozi wa uholanzi ambao walitupa anuani za mawasiliano na Elaine na Mejah walisaini. Walisema fedha hiyo itawekwa benki jumatatu. Fedha hizi zitatumika kukodisha vyombo vya muziki, mahema, kununua kofia za helimet 20 na majaketi, 20 kama zawadi na matangazo kwenye magazeti.

Wanachama walipendekeza magazeti ya Dar leo na Mtanzania Daima ili kuweka matangazo yetu. Dominata alisema ataitisha mkutano na waandishi wakati wa wiki na kuwasiliana na waandishi wa habari ili kuchapisha tukio hilo kabla na baada.

Sosthenes alisema kwamba ametengeneza bango la matangazo yeye na Juma watayaweka siku ya jumapili.

Wakati wa wiki wajumbe wengi hasa Juma na Paulo wamesambaza vipeperushi vingi. Elaine alitoa mabango na vipeperushi vyakusambaza wiki hii.

Meja alimwambia Elaine atatuatilia vyombo vya muziki na mahema pale music may day. Atatengeneza Tshirt 25 ambazo zitagawiwa wanachama wa UWABA waliohudhuria mikutano mara zote bure.

Wakati wa wiki Juma alikusanya chupa za maji 600 kutoka kampuni ya Bakhresa na kuyapeleka kwa Elaine kwa pick-up.

Guta halijakamilika lakini litakuwa tayari wiki hii.

Eline aliandaa tiketi za bahati nasibu na atazichapa wiki hii. Atachapa pia vipeperushi vya maelezo kwa washiriki.

Manispaa ya Ilala ilikubali kupitia simu tutumie Mnazi Mmoja bure. Juma atafuatilia barua kutoka manispaa ya Ilala ya kuthibitisha hili siku ya Jumatatu. Pia siku hiyo atapiga simu kwa Azan Zungu kumkumbusha kuhusu tukio.

Elaine atapiga simu Ultimate Security kuwakumbusha kuhusu gari la wagonjwa (ambulance)

Wanachama walimtaka Elaine aandae ratiba ya tukio

Dominata alisema tunatakiwa tuwape taarifa polisi na askari wa usalama barabarani. Elaine ataandika barua na Juma ataipeleka. Tutaandika pia barua ya asante kwa ubalozi wa uholanzi.

Juma alipeleka maneno ya matangazo kwenye ofisi za Clouds FM Elaine atafuatilia kwa simu kuwakumbusha kuyatoa matangazo hayo.

Tunanunua kipaza sauti (megafoni) ya nyongeza kwa ajili ya kutolea matangazo wakati wa msafara.

Wakati wa wiki Mussa Athuman na Juma walikwenda keko kuchukua guta. Siku ya msafara Ally Mohammed atawapitia wanachama wa UWABA waishio mabibo saa moja asubuhi ili waje kama kundi hadi Mnazi Mmoja wakiwa na vibendera kwenye baiskeli zao. Jumanne, sudi saidi na Yusuph Juma watumia guta kubeba maji ya kunywa kutoka kwa Elaine na kuyapeleka kinondoni ambako watawasubiri washiriki kufika hapo na kuwapa maji hayo, maji yaliyosalia atapelekwa Mnazi mmoja kama sehemu ya msafara. Sosthenes atahudhuri msafara akiwa na vifaa vya muziki na kufunga mahema. Dominata na Elaine watakuwa waangalizi wa megafoni na kuwapa wanachama kutangaza wakati wa msafara CHABADA watachagua viongozi wa kuweka msafara pamoja na kwenda taratibu na kwa nafasi.

### **Mawasiliano na TANROADS**

Wakati wa wiki Juma alipeleka barua TANROADS kufuatilia mkutano wetu.

### **Guta**

Jumanne alimpa Juma Tsh 14,000 ambapo Juma alimpa Elaine Tsh 6,000 za risiti za kurudufisha na selotape.

### **Vitambulisho**

Vitambulisho zaidi vilitolewa na wanachama wanne waliomba kupewa vitambulisho.

## **Mengineyo**

Bwana Meshak ambaye ni mwakilishi wa kampuni iitwayo Tanzament wanaotoa bidhaa kutoka china alitutembelea. Alisikia kuhusu sisi kutoka kwenye magazeti wakati tulipokuwa tunafanya kampeni za guta. Alitueleza kuhusu magari ya tairi tatu yanayotumia Betri (umeme). Wanachama wa UWABA walielezea kwamba aina hii ya magari yanaweza kurekebishwa kama magari kwani yanaweza kwenda kwa haraka, yatatumia barabara ya magari na kuwa na madereva wenye leseni. Alituambia kwamba ana baikeli zenye uwezo wa kutumia umeme kupunguza mzigo kwa mtumiaji wanachama wa UWABA walisema kwamba katiba yetu inasema kwamba tunajishughulisha na baikeli zinazotumia mnyororo na pedo kwa ajili ya usafiri. Bwana meshak alisema kwamba atafanya uchunguzi kuhusu bidhaa ambazo UWABA zinaweza kuvutiwa nazo kama helimeti na vifaa vya baikeli.